BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Nne – Tarehe 17 Septemba, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

269. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kwa mujibu wa ripoti za biashara haramu za binadamu zinaonesha kuwa Zanzibar ina ongezeko kubwa la biashara haramu ya binadamu (Human trafficking) na biashara haramu ya ngono (Sex trafficking). Ripoti ya mwezi Juni, 2023 ya Ubalozi wa Marekani ni moja ya ripoti hizo zinazoonesha ukubwa wa tatizo hili hapa Zanzibar.

(a) Je, Serikali inalitambua vipi tatizo hili na ni matukio mangapi ya biashara haramu za binaadam yamewahi kuripotiwa Zanzibar.

(b) Je, ni ipi mifumo ya uchunguzi wa matukio haya ya biashara haramu za binaadam inayotumika kuchunguza na kuzuia biashara hii haramu Zanzibar.

(c) Je, ni sheria zipi zinazosaidia katika vita hii kwa Zanzibar na ni ipi khatma ya Sheria ya Kupambana na Biashara Haramu ya Binadamu.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

78. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Je, tathmini iko vipi juu ya kupungua kwa maambukizi mapya ya VVU nchini.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

136. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la

Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

(a) Tathmini iko vipi juu ya mashirikiano baina ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU) katika mapambano dhidi ya rushwa nchini.

(b) Kwa kiasi gani wananchi wamehamasika katika kuitumia ‘code number’ 113 katika mapambano dhidi ya rushwa Zanzibar.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

6. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tunaipongeza Serikali kwa hatua iliyoichukuwa ya kujenga Vituo Maalumu vya Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar katika kila Wilaya, vikiwa na lengo la kuwaondolea usumbufu wananchi wetu wa kupata huduma zilizolengwa.

(a) Ni zipi sababu zilizopelekea mlundikano wa wananchi katika Vituo vya Wakala wa Matukio ya Kijamii, Zanzibar.

(b) Ni zipi sababu zinazopelekea kuchelewa kupatikana vitambulisho vya Mzanzibari pamoja na vyeti vya kuzaliwa kwa wananchi wetu.

(c) Je, ni lini Serikali itaiondoa tarehe ya mwisho wa matumizi (Expire date) kwa vitambulisho vya Mzanzibari hasa ikizingatiwa kuwa kuna usumbufu mkubwa wa upatikanaji wake.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

274. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Wakati wa kuwasilisha Bajeti Kuu ya Serikali mwezi Juni, 2024, Serikali ilitoa maelezo yenye matumaini kuhusu kudhibiti mfumko wa bei kwa bidhaa na huduma muhimu nchini. Hata hivyo, bado ahadi hiyo haijatekelezwa ipasavyo na kupelekea maisha kuzidi kuwa magumu kwa wananchi wa kipato cha chini.

(a) Je, ni ipi takwimu sahihi ya mfumko wa bei kwa bidhaa na huduma muhimu kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

(b) Je, ni yepi malengo ya kisera juu ya mfumko wa bei kwa bidhaa na huduma muhimu nchini.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kupambana na athari za mfumko wa bei kwa kiwango cha kitaifa.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

65. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

(a) Tangu kuanzishwa kwake ni kaulimbiu ngapi na zipi zimetumika katika kuiboresha Televisheni yetu ya Taifa ya ZBC.

(b) Ni ipi kauli mbiu ya sasa.

(c) Ni kwa kiasi gani maboresho ya vipindi mbali mbali yana mshabaha na uwepo wa kauli mbiu ya muda huu.

66. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa asilimia ngapi Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) limefanikiwa katika kuonesha vipindi vyenye matukio ya ndani ya nchi (local contents) kwa sasa.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

227. MHESHIMIWA JUMA ALI KHATIB (Uteuzi wa Rais) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kuna taarifa kuwa baadhi ya wafanyakazi katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume pamoja na Kiwanja cha Ndege cha Pemba, wanafanyakazi bila ya kuwa na mikataba ya ajira.

Je, ni lini Serikali itawapatia wafanyakazi hao ajira za kudumu.

248. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza Serikali kwa ujenzi wa barabara ili kuweza kusaidia maendeleo kwa wananchi. Pamoja na pongezi hizo, lipo jambo ambao linaonekana kuleta masuali na malalamiko kwa wananchi kutokana na utofauti wa ujenzi wa barabara hasa katika ‘design’ ya mitaro ya pembeni na upana wa barabara wenyewe.

(a) Kwa nini baadhi ya barabara kuu zinazojengwa zinaonekana hazina ‘design’ ya ujenzi wa mitaro pembeni kwa ajili ya kupitisha maji na upana wake unatofautiana.

(b) Je, jambo hili halitoleta athari na kuharibu ubora na uimara wa barabara hizi zinazotumia fedha nyingi za walipa kodi wa Zanzibar.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

1. MHESHIMWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar:

Tunaipongeza Serikali kwa kutenga fungu maalumu kwa wanafunzi wanaotaka kujiendeleza na masomo ya elimu ya juu katika ngazi mbali mbali kwa kuwapatia mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Zanzibar.

(a) Ni ipi takwimu halisi ya wanafunzi waliopatiwa mikopo hiyo kwa ngazi ya Digirii ya Pili (Master) kwa vyuo vilivyopo chini ya Compus ya SUZA tokea mwaka 2020 hadi sasa, ambao bado hawajarejesha mikopo hiyo.

(b) Serikali imeandaa mikakati gani katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wote walionufaika na mikopo wanairejesha mikopo hiyo.

(c) Ni zipi hatua za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa kwa wanafunzi ambao tayari wameshamaliza masomo na bado hawajarejesha mikopo yao hadi sasa.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

52. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa vipi na kwa kiasi gani mazao yanayotokana na kilimo chetu yanapata soko katika viwanda vilivyopo sasa.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

224. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Jimbo la Nungwi ni sehemu moja wapo yenye upungufu wa umeme na kukatikakatika kwa nishati hiyo imekuwa ni tatizo kubwa na ni la muda mrefu.

(a) Je, kwa kiwango gani Wizara yako inalifahamu tatizo hilo.

(b) Kwa kuwa tatizo hilo limedumu kwa muda mrefu sasa, ni lini litapatiwa ufumbuzi.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

70. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Bila ya shaka yoyote Wizara yako imeshafanya upembuzi yakinifu wa kuweza kubaini kwa nini soko letu tegemezi la watalii kutoka nchi ya Itali limechukua muda mrefu tangu kumalizika kwa UVIKO 19.

(a) Je, ni athari zipi zimejitokeza kutokana na kukosa soko la

watalii kutoka nchini Itali.

**Wizara**(b) Ni yepi matarajio mapya juu ya kuitatua changamoto hii.

**ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

53. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Moja kati ya majukumu ya msingi ya Tanzania Bureau of Standards (TBS) na Zanzibar Bureau of Standards (ZBS) ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na usalama wa kutosha wa chakula.

Je, tathmini iko vipi juu ya uwepo wa vifaa vya teknolojia ya kisasa vyenye uwezo wa kufanya uchambuzi wa haraka wa sampuli mbali mbali za vyakula kutoka nje ya nchi na vile vinavyozalishwa nchini.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**17 Septemba, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**